

Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe inatekeleza majukumu yake kwa kufuata miongozo mbalimbali inayotolewa na Wizara ya afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto.

Sekta ya afya

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ina jumla ya vituo (21) vya kutolea huduma za afya. Vituo hivi vinamilikiwa na serikali, watu binafsi na mashirika ya dini . Vituo vya kutoea huduma za Afya vinavyomilikiwa na serikali ni 3, kituo 1 kinamilikiwa na mtu binafsi na 1 kinamilikiwa na shirika ya dini . Kati ya vituo hivyo 21, kuna hospitali 1 ya Wilaya , vituo vya Afya 5 na zahanati 15.

Huduma kwa wamama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano

Huduma za akina mama na watoto chini ya miaka mitano zinatolewa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya serikali na kituo cha Afya cha shirika la dini. Huduma zinazotolewa ni pamoja na utoaji wa chanjo mbalimbali kwa watoto na akina mama, uzazi wa mpango, uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi n.k. Pamoja na hayo vyandarua hutolewa kwa kina mama wote wajawazito katika hudhurio lao la kwanza na watoto wanaotimiza miezi 9 wakati wa chanjo ya surua ya kwanza (MRI).

Majedwali yafuatayo yanaonyesha hali ya vifo vya mama wajawazito, watoto chini ya miaka 5 na chano.

Vifo vya akina mama wajawazito na watoto

Mwaka	Akina mama wajawazito	Watoto <5
2015	18	221
2016	20	198
2017	27	186

Takwimu za vifo vya akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka 5 vinaonekana kuongezeka hii inatokana na kuimarika kwa ukusanyaji wa takwimu,kwa kuwatumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii ambapo kupitia mpango wa malipo kwa ufanisi wamepewa jukumu la kukusanya takwimu za vifo visivyo ripotiwa katika ngazi ya jamii.

Huduma za afya tiba

Huduma hizi hutolewa kwa wagonjwa wa nje na wagonjwa wa ndani. Magonjwa yanayosumbua sana wilayani ni pamoja na Malaria, Anemia, Kifua kikuu, Kuharisha n.k. Katika kushughulikia tatizo la malaria, kupitia mpango wa Taifa wa kudhibiti malaria ulianzisha programu mpya ya ugawaji wa vyandarua kwa mama wajawazito na watoto kama mbadala wa mpango wa hati punguzo uliokuwa ukitumika hapo awali, hivyo kuanzia mwishoni mwa mwezi Desemba 2016 mpango ulipo anza kutoa vyandarua kwa mama wajawazito wakati wa hudhurio la kwanza na watoto umri wa miezi tisa wakati wa chanjo ya surua ya kwanza, vyandarua viligawiwa kama ifuatavyo;

- Mwezi Desemba 2016 mama wajawazito waliorajiwa ni 1,196 waliopewa ni 161 na watoto waliorajiwa ni 1,030 waliopewa ni 114.
- Mwaka 2017 mama wajawazito waliorajiwa ni 14,416 waliopewa ni 1193 na watoto waliorajiwa ni 11860, waliopewa ni 8031,
- Mwaka 2018 hadi mwezi june mama wajawazito waliorajiwa ni 8,750 waliopewa ni 7,040 na watoto waliorajiwa ni 5,334 waliopewa ni 5,444

Pia elimu ya hamasa juu ya matumizi sahihi ya vyandarua ili kujikinga na malaria hutolewa mara kwa mara.

Huduma za rufaa, kwa wagonjwa hususani mama wajawazito zimeimarishwa kwa kufunguliwa huduma za upasuaji wa dharula katika kituo cha afya Uyovu na uwepo wa magari ya wagonjwa 5 ambayo hutowa huduma za dharula kila yanapohitajika.

Wilaya pia hutoa njia mbalimbali za uzazi wa mpango ambapo kati ya mwaka 2015 hadi june 2018 wateja wa sindano walikuwa 15,317 BTL 2,904 vipandikizi 11,652 iucd 3,225 vaswetomy 13 vidonge 4457 na Kondom 5,496.

Kwa upande wa utoaji wa huduma za kifua kikuu wagonjwa 1748 wa kifua kikuu walitibiwa kuanzia 2015 hadi kufikia june 2018.

Chanjo kuanzia mwaka 2015

AINA YA CHANJO	2015	2016	2017	2018
BCG	105%	106%	108%	89%
POLIO 3	86%	88%	96%	80%
PENTA 3	88%	90%	97%	92%
MEASLES	80%	82%	85%	86%
PCV 3	88%	90%	97%	92%
VITAMIN A	102%	98%	97%	99%
TT2+	88%	91%	94%	90%
HPV 1	-	-	-	94%

Utoaji wa chanjo mbalimbali umeimarika ikilinganishwa na miaka ya nyuma kutokana na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya huduma za afya.

Utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa afya ya msingi (MMAM) kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2018

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kuinua sekta ya afya ili kutekeleza sera ya mwaka 2015 ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Mpango MMAM umelenga kuwa na zahanati moja kwa kila kijiji na kituo cha Afya kimoja kwa kila kata.

Ujenzi wa zahanati na vituo vya afya

Ili kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati, miradi ifuatayo inajengwa na kufikia hatua mbalimbali za utekelezaji hadi sasa. Kwa mujibu wa mpango wa maendeleo ya afya ya msingi ya kila kijiji kuwa na zahanati wilaya ina jumla ya vijiji 52 ambapo mahitaji ya zahanati mpaka sasa ni 45 katika kutekeleza hili vijiji 42 vimeanza ujenzi wa zahanati na ujenzi uko katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo; misingi iliyokwisha chimbwa ni 22, iliyojengwa 11, hatua ya lenta 6, boma 1, upauaji 1,na umaliziaji 1. Aidha vijiji 3 viko kwenye hatua za kukamilisha upatikanaji wa maeneo ya ujenzi.

Vituo vya Afya vya Uyovu na Ushirombo vinaendelea na programmu ya serikali ya kuimarisha vituo vya Afya kwa kuviwezesha kuimarisha miundo mbinu ya vituo hivyo aidha kituo cha afya uyovu kilipokea jumla ya Tshs 400,000,000/= awamu ya kwanza ambapo ujenzi uko hatua za ukamilishaji na kituo cha Afya Ushirombo kimepatiwa Tshs 500,000,000/= awamu ya pili ambapo kazi za ujenzi zinaendelea.

Ukarabati wa vituo vya kutolea huduma

Ukarabati wa zahanati umekuwa ukifanyika mara kwa mara kwa kutumia fedha za malipo ya matokeo ya ufanisi (RBF) na bajeti zao za vituo kama walivyo panga. Hadi sasa vituo vya afya na zahanati zote zimekwisha pokea fedha za RBF kwa robo tatu ya mwaka 2018 na kazi za ukarabati zinaendelea kulingana na mpango kazi wa vituo.

Changamoto

- (i) Vituo vya kutolea huduma za afya ni vichache haviendani na idadi ya wakazi waliopo wilayani Bukombe.
- (ii) Upo uhaba wa watumishi wa kada mbalimbali za afya. Mahitaji ni watumishi 574 waliopo ni 313 na mapungufu ni 257. Aidha watumishi 21 wamepangwa Wilaya ya Bukombe ambapo wanaendelea kuripoti kazini.
- (iii) Uchangiaji wa gharama za matibabu kwa wananchi unakuwa mgumu kwa sababu ya umaskini.
- (iv) Kumekuwepo na upungufu wa damu salama katika vituo vyenye mahitaji ya kutumia damu hususani wakati wa kuwasaidia mamawajawazito na watoto.

- (v) Kutokana na upungufu wa baadhi ya dawa, vifaa tiba na watumishi, kumekuwepo na malalamiko ya wateja kwa kutoridhika na huduma wanazopata.

Mikakati ya kukabiliana na changamoto

- (i) Ujenzi wa zahanati kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ambapo serikali imeweka malengo ya kuwa na zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata itongeza idadi ya vituo vya huduma na hivyo kuwasogezea wananchi huduma.
- (ii) Kupitia mpango wa MMAM tunatarajia ongezeko la idadi ya watumishi
- (iii) Kutokana na malalamiko na kero wanazopata wateja, idara imeweka masanduku na namba za simu za viongozi ngazi ya wilaya ili wananchi kupitia masanduku na namba za simu waweze kupata ufumbuzi wa kero zao kwa haraka.

Majukumu ya idara

Idara ya Afya inatekeleza majukumu makuu mawili abayo ni Afya kinga na Afya tiba. Kupitia Afya tiba idara imelenga kutoa matibabu sahihi kwa gharama nafuu kwa wananchi wa Wilaya ya Bukombe pamoja na Wilaya za jirani. Afya kinga imelenga kuwakinga wananchi wasipate magonjwa yale ya kuambukiza, yasiyoyakuambukiza pamoja na kuzuia magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu.

A: Afya tiba

Idara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufuata miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na kutekeleza mpango mkakati wa afya kwa mwaka 2015 -2020. Katika kuhakikisha wananchi wanapata tiba sahihi, idara imekuwa ikitekeleza majukumu yafuatayo:

- Kusimamia manunuzi ya dawa, vitendanishi vya maaabara ,vifaa na vifaa tiba kisha kuvisambaza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.
- Kutoa huduma za matibabu na uuguzi kupitia vituo vya kutolea huduma za Afya zikiwemo huduma za upasuaji mkubwa na mdogo. Huduma hizi ni kwa wagonjwa wa nje na wagonjwa wa kulazwa.
- Kufanya ukaguzi wa dawa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya
- Kusajili na kuhuisha maduka ya dawa na vipodozi, kuyafanyia ukaguzi mara kwa mara na kuhakikisha yanafuata sheria, kanuni na miongozo inayosimamia uanzishaji na uwepo wa maduka hayo
- Kusimamia pamoja na kuzikagua maabara zote na kuhakikisha zimesajiliwa na zinatoa huduma bora kulingana na miongozo iliyotolewa na Wizara ya Afya.
- Kutoa, kusimamia na kuratibu huduma za afya ya uzazi na mtoto katika Wilaya . Huduma hizi ni pamoja na uzazi salama, huduma za uzazi wa mpango, huduma za chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito, uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi pamoja na matiti. Huduma nyinezo ni pamoja na huduma za kuzuia ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.
- Kuratibu huduma za kuzuia maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na UKIMWI. Huduma zitolewazo ni pamoja na matibabu na matunzo kwa watu wanaoishi na virusi vya

UKIMWI, huduma za kuzuia maambukizi toka kwa mama kwenda kwa mtoto, huduma za kuchunguza na kutibu magonjwa ya ngono pamoja na huduma za wagonjwa majumbani. Huduma hizi hutolewa katika vituo vya kutolea huduma za Afya.

B: Afya kinga

Idara imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali yanayolenga kuwakinga wananchi na magonjwa ya kuambukiza. Majukumu hayo ni pamoja na:

- Ukaguzi wa nyumba za kuishi na majengo ya biashara kama vile nyumba za kulala wageni, majengo ya kutengeneza na kuuza vyakula ili kuondoa machukizo yanayoweza kuhatarisha afya ya binadamu.
- Utoaji wa elimu ya afya kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya afya.
- Utoaji wa chanjo kwa magonjwa ya kuambukiza.
- Usimamizi wa afya na usalama mahala pa kazi
- Usimamizi wa usafî wa Mazingira.